Hadithi Ya Fisi Mvivu aitwaye Masika

Swahili

Hadithi Hadithi,

Hadithi njoo, uwongo njoo, utamu kolea.

Hapo zamani za kale palikuwa na Fisi aitwaye Masika. Masika alikuwa ni Fisi mvivu sana asiyependa kufanya kazi ya aina yoyote, alipenda tu kulala muda wote. Tangia enzi zake alivyokuwa anasoma shule, hakupenda kukaa darasani na kumsikiliza mwalimu. Aliwaza tu kurudi nyumbani na kulala kitandani kwake. Masika alikuwa ni mvivu kiasi kwamba mara nyingine mwalimu wake akifundisha darasani, Masika alikuwa akisinzia. Mwalimu akimuuliza kwanini anafanya hivyo alilia kwa sauti ya unyonge! “Uuuwiii, uuuwiii, nimechoka, uuuuuwiii.” Afikapo tu nyumbani alijivuta mpaka kitandani na kulala huku akikoroma. Wazazi wake walikuwa wakimtuma kutafuta kuni kwa ajili ya kupikia lakini Masika hakuweza kufanya hivyo kwa ajili ya uvivu wake, Masika alipenda sana kucheza tu na baadae akichoka analala bila hata ya kuoga.

Masika aliendelea na tabia yake ya uvivu hadi ukubwani. Hakupenda kufanya kazi na alimtegemea mke wake ndio afanye kazi na kulisha familia nzima. Kwa kuwa mke wake alimpenda sana, alivumilia na kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuitunza familia. Kipindi fulani mke wake Masika aliugua ghalfa na hali hii ilisababisha kusiwepo na chakula kabisa ndani ya nyumba yao. Mke wake akamwabia, ”mume wangu mpendwa, jamani naomba uamke hapo kitandani ukatafute kazi ili tuweze kujipatia chakula hapa nyumbani.” Masika akaijibu kwa uvivu huku akijigeuza kitandani, “Uuuwiii, uuuwiii, nimechoka, uuuuuwiii”. Siku zilipita na wote wawili walibaki wamelala kitandani. Masika alilala kwaajili ya uzembe wake na mke wake alilala kwa kuwa alikuwa ni mgonjwa. Baada ya siku nyingi kupita Masika aliona kuwa mke wake haelekei kupona ilimbidi aamke na kwenda kutafuta kazi.

Punde tu Masika alivyotoka nyumbani kwake alisikia sauti ikitoka juu kwenye miti ikiita, ”Njoo, njooo, fanya kazi upate kula”. Masika alisimama na kutazama juu ya mti nakumuona bundi mkubwa ameketi. Bundi huyu alikuwa akiitwa Mabawa na alikuwa ni tajiri mwenye mashamba makubwa hapo kijijini kwao. Alikuwa amevaa nguo nzuri zilizopendeza na miwani mikubwa aliyoitumia kwaajili ya kusoma vitabu vilivyomfundisha mengi kuhusu mambo ya dunia. Mabawa alikuwa ni bundi mwenye roho nzuri sana na alipenda kusaidia wanakijiji wenzake. Siku hii alikuwa amekaa juu ya mti akitafuta wafanyakazi wa kumsaidia kuvuna shamba lake kubwa la mahindi. Masika akamwambia Mabawa, “Uuuwiii, uuuwiii, ninanjaa, uuuuuwiii.” Mabawa akamjibu, ” Njoo, njoo mwanangu, mtu asiye fanya kazi na asile. Njoo

Hadithi Ya Fisi Mvivu aitwaye Masika

kesho asubuhi na mapema uanze kazi ili uweze kuipatia familia yako chakula". Bwana mabawa alivyoona hali mbaya ya Masika alimuonea huruma akamwambia, "Njoo, njoo mwanangu, naona kwamba una njaa sana. Njoo chukua chakula cha kuwatosha kwa muda mfupi kisha unaweza kuja kufanya kazi kwenye shamba langu".

Kesho yake Masika alichelewa kuamka kwakuwa tabia yake ya uvivu bado alikuwa nayo. Mke wake alijaribu sana kumuamsha mpaka alilazimika kumnyang'anya shuka lake alilokuwa amejifunikia. Masika alijigeuza kitandani huku akilalamika kama kawaida yake, "Uuuwiii, uuuwiii, nimechoka, uuuuuwiii."

Siku hiyo ikapita bila ya Masika kwenda kazini.

Siku chache zilizofuata njaa ilizidi na Masika alishindwa kuvumilia akalazimika kuamka na kwenda shambani kwa bwana Mabawa. Mabawa alimkanya Masika kwa tabia yake ya uvivu lakini alimsamehe pia. Masika alielekea shambani huku akitembea kwa kujivuta. Alifika na kukuta wenzake wameshaanza kazi tangu mapema na waliendelea kuvuna mahindi. Alijiunga na wanfanyakazi wengine kukata mahindi, kuyamenya, kuyapukuchua na kuyajaza kwenye magunia kisha kuyapeleka kwenye ghala. Ghala hili lilikuwa sehemu maalum ya kuhifadhia mazao mbalimbali kwa ajili ya akiba wakati wa upungufu wa chakula.

Pamoja na Masika kupata kazi hii nzuri bado alikuwa ni mvivu kiasi kwamba wakati wenzake wameshapeleka magunia matatu au manne yeye alikuwa amepeleka moja tu. Kuona hivyo Masika aliogopa kuwa bwana Mabawa asingemlipa ujira au mshahara uliolingana na wafanyakazi wenzake. Alifikiria jinsi ya kuweza kuongeza idadi ya magunia aliyopeleka ili yalingane na ya wafanyakazi wengine. Alijiambia mwenyewe, "nikisubiri wakati wafanyakazi wengine hawanioni, nitaweza kuwaibia magunia yao na kuyakimbiza upesi ghalani. Kwa mbinu hii haitanibidii kufanya kazi nyingi lakini nitaweza kupeleka magunia mengi". Wakati anawaza kufanya hivyo bwana Mabawa alikuwa akitembelea na kukagua shughuli za kuvuna shambani mwake. Masika aliogopa sana alivyomuona na akafikiri angeweza hata kupoteza kazi yake iwapo atakutwa na kosa hilo kubwa.

Akafikiria zaidi na akapata mbinu nyingine ya kuongeza idadi ya magunia. Alijiambia mwenyewe, "Baadala ya kukata mahindi, kuyamenya, kuyapukuchua; kwanini nisichukue magunzi yaliyotoka kwenye mahindi yaliyomenywa na wenzangu, kisha niyafunge vizuri kwenye magunia kisha niyapeleke kwenye ghala?" Masika aliona kuwa hii ni njia nzuri sana ya kuweza kuepukana na kufanya kazi nyingi lakini bado ataweza kupata ujira sawa na wafanyakazi wengine. Basi huku wenzake wakifanya kazi kwa bidii na kujaza mahindi kwenye magunia, Masika aliwafuata nyuma na kuokota magunzi na matakataka mengine

Hadithi Ya Fisi Mvivu aitwaye Masika

na kuyajaza kwenye magunia yake. Alijiona mjanja sana kwa kuweza kufikiria mbinu hii ya kudanganya na kuonekana kama yeye pia ni mfanyakazi bora. Jioni ilipofika magunia yote ya masika yalihesabiwa ilimwisho wa wiki aweze kupata ujira kulingana na kazi aliyoifanya.

Siku zilipita na Masika alikuwa anaendelea kuokota magunzi na uchafu mwingine na kuyapeleka kwenye ghala. Magunia yake yalihesabiwa kama kawaida na mwisho wa siku alienda nyumbani huku akiiwaza tu siku ya mwisho wa mavuno ambapo atakuja kulipwa ujira wake wa wiki nzima.

Siku ya mwisho ya kazi ya kuvuna ilifika na wafanyakazi wote kwenye shamba la bwana Mabawa walikuwa wenye furaha sana kwa kuwa walijua siku hii watalipwa ujira wao. Masika naye alikuwa mwenye furaha kubwa kwa kuwa mbinu yake ya kudangaya ilikuwa haijagundulika na bwana Mabawa wala yeyote mwingine hapo shambani. Masika aliendelea siku hiyo ya mwisho kukusanya magunzi na uchafu mwingine na kupeleka kwenye ghala.

Jioni ilipofika Masika na wanfanyakazi wote wengine wakiwa wamebeba gunia lao la mwisho, bwana Mabawa aliwasimamisha na kuwaeleza kuwa amefurahishwa sana na kazi nzuri walioifanya wiki nzima. Bwana Mabawa aliwaambia, ”Asanteni sana kwa kazi yenu nzuri. Pia ninapenda kuwataarifu kuwa ujira wenu kwa kazi zenu mzlizozifanya; Kila mmoja wenu achukue gunia alilolibeba na mpeleke nyumbani kwaajili ya chakula kwa familia zenu”. Masika alishikwa na mshituko mkubwa na masikitiko kwa kuwa alijua gunia alilolibeba lilikuwa limejaa magunzi na matakataka tu. Huku wenzake wakishangilia Masika alianguka chini na kuanza kulia kwa sauti kubwa, “Uuuwiii, uuuwiii, tutakula nini, uuuuuwiii.” Bwana Mabawa alipoona hali hii alimuuliza Masika, ”Wewe mbona unalia na hauna raha wakati wenzako wanafurahia?” Masika alishindwa kumjibu na alibaki tu akiangalia gunia lake hadi bwana Mabawa alishawishika kufungua gunia na kuangalia yaliyomo. Bwana Mabawa alipigwa na butwaa kwa kuona magunzi na uchafu mwingine kwenye gunia la Masika. Akamwambia kwa ukali, ”Kumbe hivi ndivyo ulivyokuwa ukifanya kila siku! Tabia yako ya uzembe na uvivu leo imekuponza. Kuanzia leo wewe na familia yako na wajukuu wenu wote na vizazi vyako vyote vinavyofuata mtakuwa mkila mabaki ya chakula watakacho acha wengine baada ya kushiba”.

Ndio maana mpaka leo ukimtazama fisi utamuona amelala kwa uzembe akisubiri wengine kuacha au kudondosha chakula huku akilia ” “Uuuwiii, uuuwiii, nina njaa, uuuuuwiii.”

Hadithi yetu ya fisi mvivu aitwaye Masika ndio inaishia hapo.